# Ripoti Ya Uwajibikaji

## Mashirika Ya Umma

**2015-16**



# Ripoti Ya Uwajibikaji

## Mashirika Ya Umma

## 2015-16

Kwa kushirikiana na:

THE FOUNDATION for Civil Society

Kwa msaada wa:

Mradi wa Good Financial Governance (GFG)

Unaotekelezwa na:

giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Kwa niaba ya:

Co-funded by European Union

german cooperation DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

# Yaliyomo


Orodha ya Majedwali ..... ii

Orodha ya vielelezo ..... iii

Vifupisho ..... iv

Utangulizi ..... v

Hati za Ukaguzi ..... 1

Aina ya Hati zitolewazo na CAG ..... 1

Mwenendo wa hati za ukaguzi na mapendekezo ya CAG ..... 1

Utekelezaji wa Mapendekezo ya CAG ya miaka ya nyuma ..... 2

Masuala Muhimu yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa 2015/16 ..... 3

Jambo la 1: Uwezekano wa Kuwepo kwa Deni Linalotokana na Wafanyakazi Hewa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ..... 3

Jambo la 2: Kukosekana kwa Mkataba na Uthibitisho wa Udhamini wa Serikali kwa Chuo Kikuu cha Dodoma katika mkopo wa NHIF wa Shilingi bilioni 44.29 ..... 4

Jambo la 3: Kutorejeshwa kwa Gharama za uendeshaji za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) Shilingi bilioni 1.20 ..... 4

Jambo la 4: Madeni ya Serikali kwenye mifuko ya Hifadhi za Jamii yaliyozidi Muda wa Kulipwa Shilingi trilioni 1.6 ..... 5

Jambo la 5: Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu (NBAA) kushindwa kulipa deni la NSSF Shilingi bilioni 8.93 kwa mwaka 2015/2016 ..... 7

Jambo la 6: Usimamizi Mbovu wa Taratibu za Kutoa Mikopo katika Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) ..... 7

Jambo la 7: Tatizo la Uendelevu wa Benki ya Twiga ..... 8

Jambo la 8: Ucheleweshaji na Kutopelekwa kwa Makato ya Kisheria Shilingi bilioni 26.26. 9

Jambo la 9: Mapato ya Uhifadhi wa Mizigo Bandarini kutowasilishwa kwenye Akaunti ya Benki ya TPA ..... 10

Jambo la 10: Kutofanya Kazi Kwa Mashine za Kupimia Mafuta (Fuel Flow metres) ..... 10

Jambo la 11: Bidhaa zenye Thamani ya Shilingi Milioni 450.57 kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) Hazijawasilishwa Hospitali ya Taifa Muhimbili ..... 11

Jambo la 12: Usimamizi wa Kampuni Binafsi za Uzalishaji Umeme na Gharama Zake ..... 12

Jambo la 13: Uteuzi wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma ..... 13

Hitimisho ..... 13

# Orodha Ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Mafao ya wafanyakazi na kodi ambazo hazijawakilishwa kwa wakati ........ 9

Jedwali Na. 2: Orodha ya Makampuni binafsi ya uzalishaji wa Umeme pamoja na gharama zake ........ 12

# Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Mashirika ya Umma Mwaka 2013/14 hadi 2015/16 ..... 2

Kielelezo Na. 2: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2015/16. ..... 3

Kielelezo Na. 3: Madeni ya serikali yaliyozidi muda wa kulipwa ..... 5

Kielelezo Na. 4: Deni la Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Kufikia Tarehe 30 Juni, 2014 ..... 6

Kielelezo Na. 5: Mapato ambayo hayakuwasilishwa kwenye akaunti ya TPA ..... 10

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| WAJIBU | Taasisi ya Uwajibikaji Kwa Umma |
| NBAA | Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu |
| IPSAs | Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Taasisi za Umma |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| PPF | Mfuko wa Pensheni wa PPF |
| NSSF | Mfuko wa Pensheni wa NSSF |
| LAPF | Mfuko wa Pensheni wa LAPF |
| PSPF | Mfuko wa Pensheni wa PSPF |
| WCF | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi |
| GEPF | Mfuko wa Pensheni wa GEPF |
| APC | Kituo cha Taaluma cha Uhasibu |
| TPA | Mamlaka ya Bandari Tanzania |
| TANESCO | Shirikal la Umeme Tanzania |
| NHIF | Mfuko wa Bima ya Afya |
| CHF | Mfuko wa Afya ya Jamii |
| MoU | Memoranda ya Makubaliano |
| TWB | Benki ya Wanawake Tanzania |
| KOJ | Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini |
| MSD | Bohari Kuu ya Dawa |
| EPP's | Wazalishaji wa Umeme wa dharura |
| IPP's | Wazalisha wa umeme binafsi |
| IPTL | Kampuni ya Tanzania ya kuzalisha umeme binafsi |
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| TAKUKURU | Tume ya Kuzuia na kupambana na Rushwa |

# Utangulizi



Taasisi ya WAJIBU ni taasisi fikra ya uwajibikaji wa Umma iliyoanzishwa mwaka 2015 kwa lengo la kutengeneza mazingira ya kukuza uwajibikaji na Utawala bora hapa nchini. Ili kukamilisha adhma hiyo, WAJIBU kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2015/16 ya Mashirika ya Umma imeandaa Ripoti ya Uwajibikaji katika Mashirika ya Umma. Mashirika ya Umma kisheria ni mashirika ambayo Serikali inaumiliki wa kuanzia asilimia 50. Kwa mwaka 2015/16, ripoti ya CAG inaonyesha kuwa kati ya Mashirika 200 yaliyotakiwa kukaguliwa, ni mashirika 112 tu ndiyo yalikaguliwa. Hii ni Kutokana na sababu mbalimbali ikwemo ya ufinyu wa rasilimali, mfano katika mwaka 2015/16 bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipunguzwa kwa asilimia 40.

Katika kuandaa ripoti hii ya kwanza ya uwajibikaji, WAJIBU, imeshirikiana na GIZ ambayo ni taasisi ya utekelezaji ya Ushirikiano wa Ujerumani Tanzania kupitia mradi wa Utawala bora wa Fedha za Umma (Good Financial Governance). Mradi huu unatekelezwa na GIZ kwa niaba ya Umoja wa Ulaya, Ushirikiano wa Ujerumani Tanzania, na Shirika la Maendeleo la Uswisi. Ripoti hii itakuwa inatolewa kila mwaka na itakuwa katika lugha rahisi na rafiki kwa ajili ya wananchi wa kawaida. Pia ripoti hii itachambua mapendekezo ya CAG yaliyotolewa kutokana na ukaguzi wa Mashirika ya Umma yenye umuhimu mkubwa kwa Umma.

WAJIBU inatarajia ripoti hii itaongeza uelewa wa wananchi juu ya ripoti ya CAG ya Mashirika ya Umma ya mwaka 2015/16. Pia, ripoti hii itawawezesha wananchi kudai uwajibikaji kutoka kwa watendaji wa Serikali pale watakapoona hawajawajibika ipasavyo. Vilevile, ripoti hii itafanya mapendekezo ya CAG yawe na uhai wa muda mrefu zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma, hivyo itachangia kuongeza utekelezaji wa mapendekezo hayo.

Ripoti hii imegawanyika katika sehemu Tano (5) Sehemu ya kwanza ni Utangulizi, sehemu ya pili Hati za Ukaguzi, sehemu ya tatu Utekelezaji wa Mapendekezo ya miaka ya nyuma, sehemu ya nne ni Masuala Muhimu yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa 2015/2016 na sehemu ya tano ni hitimisho.



**Ludovick S. L. Utouh**
Mkurugenzi Mtendaji
WAJIBU – Institute of Public Accountability

# Hati za Ukaguzi

Hati za Ukaguzi ni maoni ya Mkaguzi wa Hesabu kuhusu ukaguzi wa hesabu za Taasisi inayokaguliwa. Maoni haya yanaonesha kama hesabu zilizokaguliwa zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kihasibu vya kimataifa (IPSAs) na matamko yanayotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

### Aina ya Hati zitolewazo na CAG

Katika ukaguzi wa sekta ya Umma, wakaguzi hutoa hati zifuatazo;

i. **Hati inayoridhisha (hati safi):** Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu za mkaguliwa zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA).

ii. **Hati Yenye Mashaka:** Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kuwepo kwa makosa ya msingi ya kiuhasibu yanayohusu mapato, matumizi au rasilimali ya shirika linalokaguliwa.

iii. **Hati Isiyoridhisha:** Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa, taarifa za fedha na rasilimali za mkaguliwa kwa kiasi kikubwa zina makosa ya msingi ya kiuhasibu na kiutendaji pamoja na kuwepo na usimamizi mbovu wa mifumo ya udhibiti ya ndani.

iv. **Kushindwa kutoa Hati (Hati Mbaya):** Hali hii kulingana na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndiyo inayozungumziwa kama, Hati mbaya ya ukaguzi. Taarifa ya aina hii hutolewa pale ambapo mkaguzi anajiridhisha kuwa mkaguliwa hana kumbukumbu za fedha na rasilimali zinazotosheleza kutengeneza taarifa za mahesabu ya shirika pamoja na kuwepo udhaifu mkubwa wa usimamizi wa mifumo ya udhibiti ya ndani.


Katika ukaguzi wa Mashirika ya Umma, endapo shirika litapata hati isiyoridhisha au hati mbaya, wadau watapoteza imani na usahihi wa taarifa za mapato na matumizi ya shirika husika. Hali hii huondoa uwezo wa shirika kupata rasilimali nyingine ikiwemo mikopo, kupungua kwa bei ya hisa n.k

### Mwenendo wa Hati za Ukaguzi na Mapendekezo ya CAG

Ripoti ya CAG inaonesha, kati ya mashirika 112 yaliyokaguliwa, mashirika 108 sawa na asilimia 96 yalipata Hati Zinazoridhisha, mashirika 4 sawa na asilimia 4 yalipata Hati Zenye Shaka, hakuna shirika liliyopata Hati Isiyoridhisha wala Hati Mbaya. Ili kujua aina ya hati zilizopatikana katika mashirika ya Umma pitia ripoti ya CAG ya Mashirika ya Umma ya mwaka 2015/16 inayopatikana katika tovuti ya http://www.nao.go.tz. Kadhalika, mwenendo wa hati za ukaguzi kwa Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na.1 hapo chini.

**Kielelezo Na. 1:**

**Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Mashirika ya Umma Mwaka 2013/14 hadi 2015/16**




**Utekelezaji wa Mapendekezo ya CAG ya miaka ya nyuma**

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za miaka iliyopita, CAG alibaini kwamba, kati ya mapendekezo 53 yaliyotolewa ni mapendekezo 39 (sawa na asilimia 74) ndiyo yametekelezwa na hivyo kubaki na mapendekezo 14 (sawa na asilimia 26) yakiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Hali hii inaoneshwa kwenye kielelezo Na. 2 hapo chini;

Utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kuhusu Mashirika ya Umma pamoja na masuala mengine unaathiriwa na yafuatayo:


1. Kutokuwepo na mfumo wa kuratibu utekelezaji wa mapendekezo haya chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na Bunge.

2. Kutowajibika ipasavyo kwa Bodi za Mashirika na Menejimenti.

3. Kutokuwepo kwa bajeti za utekelezaji wa mapendekezo ya CAG katika Mashirika ya Umma.

**Kielelezo Na. 2:**

**Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2015/15**




## Masuala Muhimu yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa 2015/16

WAJIBU katika kuifanyia uchambuzi ripoti ya ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine ya mwaka 2015/16, imejikita zaidi kwenye yale masuala muhimu na yenye maslahi makubwa zaidi kwa umma, pamoja na mapendekezo ya nini kifanyike ili kutoa ufumbuzi wa masuala hayo.

## Jambo la 1: Uwezekano wa Kuwepo kwa Deni Linalotokana na Wafanyakazi Hewa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Katika mwaka 2015/16, Serikali ilianzisha kikosi kazi kwa ajili ya kufanya zoezi maalum la kuwatambua wafanyakazi hewa katika taasisi mbalimbali za Serikali. Wafanyakazi hewa waliotambuliwa walikuwa katika mfumo wa malipo ya mshahara wa taasisi hizi. Kwa utaratibu wa utayarishaji wa mishahara, kisheria unaambatana na ukokotoaji wa makato ya lazima ambayo yanawasilishwa kwa taasisi husika kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mifuko mbali mbali ya Hifadhi za Jamii kama NSSF, PPF, PSPF, LAPF nk. Hivyo, kuna uwezekano mkubwa kuwa michango hiyo itakuwa imepelekwa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kimakosa kwa kuwa kiuhalisia michango hii haina wenyewe. Kaguzi za mifuko ya hifadhi ya jamii zimebaini kuwa mifuko hii bado haijapokea majina na taarifa za wafanyakazi hewa kutoka Hazina ili ziweze kukokotoa fedha zilizolipwa kwao kimakosa; na kuwa hadi sasa hakuna uhakiki binafsi uliofanywa na menejimenti za mifuko hii ili kubaini kiasi cha deni linalotokana na michango ya wafanyakazi hewa.

**Athari:** Kutokana na kuwepo kwa wafanyakazi hewa, ni dhahiri kuwa Serikali imelipa malipo ambayo hayakustahili kulipwa katika Mifuko ya Hifadhi na Mamlaka ya Mapato. Fedha hizi zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo ya Taifa.

**Pendekezo:** Hazina watumie taarifa walizonazo za watumishi hewa ili kubaini ni kiasi gani cha makato ambayo hayakustahili kulipwa kwa Mifuko Ya Hifadhi Ya Jamii na Mamlaka ya Mapato kwa madhumuni ya kutaka fedha hizo zirejeshwe Serikalini.

## Jambo la 2: Kukosekana kwa Mkataba na Uthibitisho wa Udhamini wa Serikali kwa Chuo Kikuu Cha Dodoma Katika Mkopo wa NHIF wa Shilingi Bilioni 44.29

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulitoa mkopo wa Shilingi bilioni 44.29 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya cha Chuo Kikuu cha Dodoma. Hata hivyo, imebainika kuwa, mkopo huo haukuwa na mkataba wala uthibitisho wa udhamini kutoka serikalini. Kuwapo kwa mkataba kungesaidia kuweka wazi haki na wajibu wa kila upande katika mkopo huu na utaratibu wa riba na urejeshaji wa mkopo.

**Athari:** Kukosekana kwa mkataba na uthibitisho wa udhamini wa serikali kunaweza kuusababishia mfuko kupoteza fedha za wanachama endapo mkopaji atashindwa kuwa mwaminifu, na itakuwa vigumu kupata haki mahakamani.

**Pendekezo:** Menejimenti ya NHIF inashauriwa kuhakikisha mkataba wa mkopo unaingiwa kati yake na mkopaji. Pia, uthibitisho wa udhamini unapatikana kutoka Serikalini. Aidha, NHIF inashauriwa kuhakikisha kuwa, mikataba halali ina kuwepo kabla ya kutoa mkopo wowote hapo mbeleni.




## Jambo La 3: Kutorejeshwa kwa Gharama za Uendeshaji za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) Shilingi Bilioni 1.20

Mfuko wa Bima ya Afya ulisaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiitaka Serikali kutoa fedha kwa ajili ya kuuendesha Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF). Katika makubaliano hayo, NHIF ilipaswa kutoa fedha za kugharamia shughuli za kawaida za uendeshaji wa Mfuko huo. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2015, NHIF ilipaswa kuwa imerejeshewa na Serikali Shilingi bilioni 1.20 kutokana na gharama

iliyotumia kwenye miradi ya CHF kama ilivyoainishwa kwenye Hati ya Makubaliano. Hata hivyo, gharama hizo hazikuweza kurejeshwa na Serikali.

**Athari:** Kwa Serikali kushindwa kulipa kumeipunguzia NHIF uwezo wa kifedha na kunaweza kuisababishia kushindwa kuhudumia wanachama wake. Pia, hali hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na kushindwa kupanua wigo wa shughuli zake.


**Pendekezo:** Menejimenti ya NHIF inashauriwa kuchukua hatua za ziada ili kuhakikisha Serikali inarejesha fedha husika.

## Jambo la 4: Madeni ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii Yaliyozidi Muda wa Kulipwa Shilingi Trilioni 1.6

Serikali inakopa kutoka taasisi mbalimbali za umma, pia inadhamini mashirika mengine kukopa katika taasisi za umma kwa kuwa ina wajibu kisheria kufanya hivyo. Kwa mantiki hiyo, Serikali inachukua jukumu la madeni hayo yanayotakiwa kulipwa kulingana na matakwa ya kisheria na kimkataba kama walivyokubaliana. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 imebainika kwamba, serikali inadaiwa madeni ya shilingi trilioni 1.60 yaliyozidi muda wake wa kulipwa kutoka katika taasisi tofauti kumi na tisa (19). Madeni haya yanatokana na mikopo ya moja kwa moja, dhamana, na michango ambayo haikuwasilishwa kulingana na matakwa ya sheria.

**Kielelezo Na. 3:**


**Madeni ya serikali yaliyozidi muda wa kulipwa**





Deni hili la Serikali kwa mifuko ya hifadhi ya jamii linaonekana kukua kwa kasi ukilinganisha na miaka ya nyuma. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2014 deni la Serikali kwa Mifuko lilifikia kiasi cha Shilingi za Kitanzania Trilioni 1.698 ambapo Shilingi za Kitanzania bilioni 975.05 sawa na asilimia 57 zilipaswa ziwe zimekwishalipwa lakini bado hazijalipwa

**Kielelezo Na. 4:**

**Deni la Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Kufikia Tarehe 30 Juni, 2014**




**Athari:** Kutokulipwa kwa madeni hayo kwa taasisi husika kunaathiri uwezo wa kifedha wa taasisi zinazotarajia kupokea fedha hizo; Kwa upande mwingine, kunaathiri shughuli zao za kiutendaji.



**Pendekezo:** Serikali inashauriwa kufanya juhudi za makusudi kuokoa hali ya kifedha kwenye Mifuko hiyo kwa kulipa madeni hayo; kwani baadhi ya taasisi zimedhoofika kifedha kiasi kwamba haziwezi kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu na kwa ufanisi unaotakiwa.

## Jambo la 5: Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu (NBAA) Kushindwa Kulipa Deni la NSSF Shilingi Bilioni 8.93 kwa Mwaka 2015/16

Tarehe 1 Novemba 2010, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu (NBAA) iliingia mkataba na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kupewa mkopo wa Shilingi bilioni 15 wenye asilimia 100 ya dhamana ya Serikali kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Taaluma ya Uhasibu (APC). CAG aligundua kuwa Bodi imeshindwa kusimamia ulipaji wa mkopo huo kwa kuwa mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2016 ilikuwa inadaiwa Shilingi bilioni 8.93.

**Athari:** Kuchelewa kulipwa deni hili kunakwamisha baadhi ya shughuli za maendeleo zinazofanywa na NSSF. Kuna hatari ya NSSF kushindwa kulipa mafao ya wanachama wake, hii ni kwasababu NSSF ikiwa kama mfuko wa hifadhi ya jamii, inatakiwa kuendelea kuwekeza fedha za wanachama wake ili kuweza kulipa mafao ya wanachama wake pale watakapo staafu.

**Pendekezo:** Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu (NBAA) inashauriwa kufikia muafaka na NSSF kuhusu ongezeko la muda wa kulipa deni hilo na kulifanya jengo la APC liwe la kibiashara ili kuweza kuzalisha fedha za kulipa mkopo huo.

## Jambo la 6: Usimamizi Mbovu wa Taratibu za Kutoa Mikopo Katika Benki ya Wanawake Tanzania (TWB)

Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) imekuwa na usimamizi mbovu wa utoaji wa mikopo. Kuna taratibu ambazo mkopaji anatakiwa kuzitimiza kabla ya mchakato wa kutoa mkopo kuanza. Pia, benki inatakiwa kuhakikisha vibali na uidhinishaji katika ngazi zote unazingatiwa ikiwa ni pamoja na tathmini ya dhamana zilizowekwa na mkopaji. Taratibu hizi zinafanywa ili kulinda maslahi ya benki na kuzuia vitendo vyovyote vya udanganyifu ambavyo vinaweza kufanywa na mkopaji. Ukaguzi wa utendaji wa benki kwa mwaka wa fedha 2014/15 umebaini hitilafu zifuatazo zinazohusiana na usimamizi wa mikopo na nyaraka.

i. Mikopo yenye jumla ya Shilingi milioni 655.00 imetolewa kwa makampuni manne bila kuthibitisha uwepo wa makampuni hayo kwa Msajili wa Makapuni.


ii. Mkopo wa shilingi milioni 200 uliotolewa kwa mteja mmoja bila dhamana kwa mwaka wa fedha 2014/15 tofauti na matakwa ya miongozo ya utoaji mikopo.

iii. Mikopo ya Shilingi milioni 330 iliyotolewa kwa wateja wanne (4) bila kuthaminisha mali.

iv. Mikopo ya shilingi milioni 355 imetolewa kwa wateja sita (6) ambao leseni zao za biashara zimemalizika muda wake wa matumizi.

v. Mikopo ya waajiriwa (salary loans) ya shilingi milioni 134 imetolewa kwa waajiriwa watano (5)

bila kuwa na uthibitisho wa udhamini (guarantee) kutoka kwa waajiri. Aidha, imebainika kuwa katika wateja waliokopeshwa, wanne (4) kati yao ni wafanyakazi wa benki za NMB, NBC na Barclays Tanzania.




**Athari:** Mapungufu katika nyaraka yanaweza kusababisha benki ikashindwa kurejeshewa fedha ilizokopesha. Pia, inaonesha kuna viashiria vya rushwa katika utoaji wa mikopo kwa kuwa ni vigumu sana kwa wafanyakazi wa benki moja kuchukua mkopo kutoka benki nyingine bila uthibitisho wa udhamini kutoka kwa waajiri wao.

**Pendekezo:** Menejimenti ya TWB inashauriwa kuboresha udhibiti katika utoaji mikopo kwa kuhakikisha nyaraka na hatua zote muhimu zinafanyika kabla ya uidhinishaji wa mikopo. Pia, tahadhari zaidi zinahitajika kuchukuliwa dhidi ya mikopo iliyotolewa kwa wakopaji wote wa benki ili kuhakikisha, pamoja na mambo mengine kama kweli.

## Jambo la 7: Tatizo la Uendelevu wa Benki ya Twiga

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2014, benki ya Twiga ilipata hasara ya shilingi bilioni 13.08. Pia kwa mwaka wa fedha ulioishia 31 Desemba 2015, benki ya Twiga ilipata hasara ya Shilingi bilioni 3.4. Aidha, katika mwaka ulioishia 31 Desemba 2014, benki ilikuwa na upungufu wa mali ya wana hisa (Equity) shilingi bilioni 20.62. Mwaka unaoishia 31 Desemba 2015, benki ilikuwa na upungufu wa mtaji kwa wana hisa wenye thamani ya Shilingi bilioni 18.7. Aidha, mtaji wa msingi wa benki katika miaka miwili ni chini ya kiwango cha chini kinachohitajika cha thamani ya shilingi bilioni 5 kama kinavyosomeka kwenye kifungu cha 17 cha Sheria ya Benki na taasisi za fedha. Pia, sheria hii inahitaji benki kuhakikisha kwamba, nyakati zote inakuwa na mtaji wa msingi usiopungua asilimia 10 na mtaji wa jumla usiopungua asilimia 12.

**Athari:** Hali hii inaleta mashaka juu ya uwezo wa benki hii kuendelea kujiendesha kwa faida, pia wateja wenye fedha zao kwenye benki hii watakosa imani na usalama wa fedha zao

**Pendekezo:** CAG katika ripoti yake anaishauri menejimenti ya benki kufanya uchunguzi na kuainisha sababu zilizopelekea benki kufanya vibaya. Pia, kubuni mikakati itakayo wezesha kuokoa utendaji wa benki.

## Jambo la 8: Ucheleweshaji na Kutopelekwa kwa Makato ya Kisheria Shilingi bilioni 26.26

Tathmini ya makato ya kisheria kwa mujibu wa ripoti ya CAG ilibaini kwamba baadhi ya mashirika hayakupeleka makato yake kwa muda uliowekwa. Makato hayo ya kisheria ambayo hayakupelekwa yanajumuisha michango ya kodi ya VAT, PAYE, michango ya pensheni pamoja na kodi ya ujuzi na maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 26.26. Madeni haya yameendelea kuongezeka kwa miaka kadhaa. Hali hii inaweza kupelekea kulipa faini, riba, na adhabu ambazo zitaathiri hali ya kifedha ya mifuko; hivyo kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa.

**Jedwali Na. 1: Mafao ya wafanyakazi na kodi ambayo hayajapelekwa kwa wakati**

| Taasisi | Kodi (VAT & PAYE) 'Shilingi bilioni' | Mifuko ya Pensheni 'Shilingi bilioni | SDL 'Shilingi bilioni | Jumla 'bilioni' |
|---|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Maji Safi na Taka Songea | 0.07 | 0 | 0 | 0.07 |
| Chuo Huria Tanzania | 3.64 | 0.44 | 0 | 4.08 |
| Shirika la Posts Tanzania | 10.58 | 0 | 3.77 | 14.35 |
| DAWASCO | 2.95 | 1.17 | 2.72 | 6.84 |
| Ushirika wa Soko Kariakoo | 0.37 | 0 | 0.27 | 0.64 |
| Mamlaka ya Maji Safi na Taka Lindi | 0.06 | 0.09 | 0 | 0.15 |
| Mamlaka ya Maji Safi na Taka Tanga | 0 | 0 | 0.12 | 0.12 |
| **Jumla** | **17.68** | **1.70** | **6.88** | **26.26** |


**Athari:** kutokulipwa kwa kodi kunaathiri kiasi cha mapato ambayo Serikali ingepata. Pia, kutolipa michango ya pensheni kwa wakati kunaathiri uwezo wa Mifuko kulipa mafao kwa wanachama wake.

**Pendekezo:** Menejimenti za taasisi hizo zinashauriwa kuchukua hatua stahiki za kisheria ili kuhakikisha makato yote ya kisheria yanapelekwa kwenye taasisi husika kwa wakati. Hali hii itasaidia kuepuka faini, riba na adhabu zisizokuwa za lazima.

## Jambo la 9: Mapato ya Uhifadhi wa Mizigo Bandarini kutowasilishwa kwenye Akaunti ya Benki ya TPA

Kwa mujibu wa ripoti ya CAG, aya E (ii) ya Memoranda ya Makubaliano (MOU) kati ya TRA na TPA, inaitaka TRA baada ya kukusanya mapato ya kuhifadhi mizigo bandarini kuyawasilisha kwenye akaunti ya benki ya Mamlaka ya Bandari ndani ya siku 14. Hata hivyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibaini kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 98.7 kilichokusanywa na TRA kati ya mwezi Agosti hadi Disemba mwaka 2016 hakikuwasilishwa kwenye akaunti ya TPA kama makubaliano yanavyotaka. Kielelezo kifuatacho kinaonesha mchanganua wa kiasi hicho:

**Kielelezo Na. 5: Mapato ambayo hayakuwasilishwa kwenye akaunti ya TPA**





**Athari:** Kutowasilishwa kwa makusanyo haya kwenye akaunti ya TPA kunaleta viashiria vya uwepo wa matumizi mabaya ya fedha hizo.

**Pendekezo:** TRA inatakiwa kutekeleza matakwa ya Memoranda ya Makubaliano inayowataka kuwasilisha makusanyo yote ya mizigo kwenye akaunti ya TPA

## Jambo la 10: Kutofanya Kazi Kwa Mashine za Kupimia Mafuta (Fuel Flow meters)

Katika ripoti ya CAG inabainishwa kuwa, gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini (KOJ) ina mashine 16 za kupimia mafuta na zote hazifanyi kazi kwa muda mrefu. Mapitio ya metriki tani zilizotolewa kutoka katika kituo cha KOJ yalibaini kuwa wastani wa 202,476.76 metriki kwa mwezi (kwa miezi ya Agosti 2015, oktoba 2015 Machi 2016) zilitolewa kupitia kituo cha KOJ bila ya kupitia kwenye mashine za kupimia mafuta kwa sababu mashine hizo zilikuwa hazifanyi kazi.




**Athari:** Kutokuwapo kwa mashine za kupimia mafuta kunapelekea kutokuwa na usahihi katika utozaji kodi wa mafuta yaliyohifadhiwa; hivyo, kupelekea kupotea kwa mapato ya Serikali.

**Mapendekezo:**

a) Kuna umuhimu wa Mamlaka ya Mapato, Mamlaka ya Bandari na Wakala wa Vipimo wakae kwa pamoja ili kupata ufumbuzi wa kudumu utakaowezesha hizo mashine za kupimia mafuta zifanye kazi muda wote kwa manufaa ya taifa

b) Kujadiliana na serikali ili Mamlaka iweze kutumia hifadhi za matanki ya TIPER ili kupunguza umbali kati ya meli na vituo vya mafuta, hivyo kupunguza siku ambazo meli itakaa na kutia nanga bandarini;

c) Kutekeleza ujenzi wa kituo cha hifadhi ya mafuta kama ilivyopangwa ili kuboresha menejimenti ya mfumo wa uhifadhi mafuta;

## Jambo la 11: Bidhaa zenye Thamani ya Shilingi Milioni 450.57 kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) Hazijawasilishwa Hospitali ya Taifa Muhimbili

Mapitio ya ankara kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) yameonesha kuna ankara 48 zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.29 zililipiwa na Hospitali ya Muhimbili tangu mwaka 2010. Hata hivyo, imebainika kuwa bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.84 ndizo zimefika na kupokelewa na Hospitali ya Taifa Muhimbili mpaka kufikia Juni 2016, na kuacha bidhaa zenye thamani ya Shilingi milioni 450.57 zikiwa hazijafikishwa katika Hospitali ya Muhimbili.

**Athari:** Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha dawa ambazo hazijapelekwa hospitalini pamoja na muda mrefu kupita ni dalili za kuwepo kwa wizi, ubadhirifu ama rushwa kati ya watendaji wa Bohari kuu ya dawa na Hospitali husika

**Pendekezo:** Menejimenti ya Muhimbili ishirikishe taasisi za uchunguzi kama TAKUKURU, Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali katika kuchunguza suala husika na kufanya usuluhishi wa taarifa na MSD na kufuatilia bidhaa ambazo hazijapokelewa.

## Jambo la 12: Usimamizi wa Kampuni Binafsi za Uzalishaji Umeme na Gharama Zake

Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) limeingia mikataba na makampuni binafsi matano yanayozalisha umeme. Ripoti ya CAG inaeleza kuwa, Shirika linanunua umeme kwa bei ya wastani wa Shilingi 544.65 kwa kila uniti na kuuza kwa Shilingi 279.35. Hivyo, kwa kila uniti moja, shirika linapata hasara ya Shilingi 265.3 kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 2: Orodha ya Makampuni binafsi ya uzalishaji wa Umeme pamoja na gharama zake**

| Kampuni | Aina ya mafuta | Uwezo MW | Mtambo (%) | Bei ya Umeme (US$/kWh) | Gharama za uzalishaji (US$/Mon) |
|---|---|---|---|---|---|
| ***Wazalishaji wa Umeme wa dharura (EPP's)*** | | | | | |
| Aggreko | Petroli | 100 | 75 | 0.38 | 1,806,255 |
| Symbion 112 | Mafuta ya ndege | 112 | 75 | 0.38 | 2,827,283 |
| Symbion Dom & Arusha | Petroli | 105 | 75 | 0.39 | 3,779,213 |
| ***Wazalisha wa umeme binafsi (IPP's)*** | | | | | |
| Songas-Gas | Gesi asilia | 189 | 92 | 0.03 | 5,266,169 |
| IPTL (Interim) | Mafuta Mazito | 100 | 75 | 0.23 | 2,678,233 |

CAG anaeleza kuwa, kabla ya kusitishwa kwa mkataba na Symbion, TANESCO ilikuwa inalipa jumla ya Dola za Marekani milioni 16.36 kama gharama za umeme (capacity charges) kwa makampuni matatu yanayozalisha umeme wa dharura na mawili ya binafsi kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo juu. Kwa sasa, Shirika linatumia Dola za Marekani milioni 9.75 kwa mwezi kununua umeme kutoka Aggreko, Songas na IPTL gharama za umeme zinazolipwa na TANESCO kwa mwezi ni Dola za Marekani milioni 9.75.

**Athari:** Shirika litashindwa kutoa huduma kwa wananchi, vilevile shirika litashindwa kuendesha shughuli zake, na kupelekea wananchi kukosa huduma na kudhoofisha shughuli za maendeleo.

**Pendekezo:**

a) Bei za umeme zinazopitishwa na EWURA zizingatie gharama halisi zinazotumiwa na TANESCO kuzalisha umeme au kununua toka kwa makampuni binafsi ya uzalishaji umeme. Vile vile, bei itakayopitishwa izingatie gharama za uendeshaji wa shirika na uwezo wa kufanya uwekezaji kwenye miundombinu ili huduma ya umeme iendelee kuwa endelevu.

b) Manunuzi ya umeme toka kwenye makampuni binafsi ya uzalishaji umeme yafanywe kwa uwazi na ushindani kama inavyotakiwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 ili kuwezesha TANESCO kupata bei nafuu.

c) Serikali iwekeze zaidi kwenye gesi ili iwezeshe TANESCO kuzalisha umeme mwingi na wa bei nafuu zaidi.

## Jambo la 13: Uteuzi wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma

Kwa mwaka 2015/16, CAG aligundua kuwa kulikuwa na Bodi za mashirika 18 ambazo zilikuwa zimemaliza muda wake; na hakuna Bodi mpya za kusimamia mashirika hayo zilikuwa zimeteuliwa hadi ukaguzi huu ulipokuwa unakamilishwa mwezi Machi, 2017. Baadhi ya taasisi hizi zimekuwa zikiendelea na utendaji wa kazi zao bila ya kuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi kwa zaidi ya kipindi cha mwaka mmoja. Mfano bodi ya Katani (TSB), Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Chama cha haki miliki Tanzania (COSOTA), Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Rufiji (RUBADA) n.k.

**Athari:** Kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi au Wadhamini wa Mashirika ya Umma kunazorotesha shughuli za kiutendaji za mashirika hayo ikiwa ni pamoja na kupitisha hesabu, bajeti na sera za utendaji wa Taasisi husika.

**Pendekezo:**

a) Serikali iteue Bodi za Wakurugenzi au Wadhamini kwa wakati pindi Bodi hizo zinapomaliza muda wake ili ziweze pamoja na mambo mengine, kupitia taarifa za mahesabu kwa muda muafaka ili kuwezesha mchakato wa ukaguzi kuendelea na kukamilika kwa wakati.

b) Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamizi mkuu wa Mashirika ya Umma aandae utaratibu utakaomuwezesha kutambua ni lini kipindi cha Bodi za Mashirika ya Umma zitakapofikia kikomo. Hii itamuwezesha kuzikumbusha Mamlaka za uteuzi wa Bodi hizo kuanza mchakato wa uteuzi mapema (ikiwezekana miezi 6 kabla ya Bodi kumaliza muda wake) kwa utaratibu huu utachangia kupunguza tatizo hili kwa kiasi kikubwa.

## Hitimisho

WAJIBU inaamini kuwa kwa taasisi zinazohusika na Uwajibikaji pamoja na wananchi wakizielewa vizuri ripoti za CAG, itachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza uwajibikaji na utawala bora hapa nchini. WAJIBU inategemea itakuwa rahisi kwa wananchi wa kawaida kusoma na kulielewa chapisho hili na mengine ya ripoti ya CAG ya ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ambayo yametengenezwa na kusambazwa na WAJIBU kwa kushirikiana na wadau wengine kama GIZ.

Kuna umuhimu kwa Serikali na wadau wengine wote wakijumuishwa Wananchi kuhakikisha kuwa mapungufu na mapendekezo yaliyotolewa na CAG yanafanyiwa kazi kikamilifu. Hii itaongeza ufanisi wa shughuli za Mashirika ya Umma na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo ya nchi na hatimaye mwananchi mmoja mmoja.

WAJIBU itashukuru sana kupata mrejesho kutoka kwa wasomaji wa chapisho hili kuhusu namna ya kuliboresha na kulifanya liweze kukuza uwajibikaji nchi nzima.

**WAJIBU - Institute of Public Accountability**
P. O. Box 13486 Dar Es Salaam
Barua pepe: admin@wajibu.or.tz ; Simu: +255 22 266 6916
Tovuti: www.wajibu.or.tz